

Nasi tunapata wokovu kwa sababu Yesu alishinda dhambi na akapeana maisha yake yasiyokuwa na dhambi kama dhabihu. Sasa Yesu anaweza kutuomba kwa Mungu ili atusamehe dhambi zetu. Yesu anaelewa wakati tunajaribiwa. Anajua ugumu wa kushindana na dhambi. Yesu huwa anatusaidia kwa sababu anajua na anaelewa vile tunajisikia.

### Maswali na Majibu

1. Taja watu 4 wenye Mungu aliahidi na Yesu akaja kutimiza.  
*Adamu, Ibrahimu, Daudi, Sedekia*
2. Jina Yesu Kristo lina maana gani?  
*Yesu inamaanisha Mwokozi. Kristo linamaanisha Mfalme. Yesu Kristo ni Mwokozi Mfalme.*
3. Yesu ni Mwana wa Mungu namna gani?  
*Alizaliwa na Mariamu kupitia kwa nguvu za Roho Mtakatifu.*
4. Yesu ni Mwana wa binadamu namna gani?  
*Alizaliwa na Mariamu aliyekuwa mzao wa wale walioahidiwa.*
5. Yesu ni Mungu Mwana? Ni mara ngapi Biblia imetaja Mungu Mwana?  
*Hapana Yesu si Mungu Mwana. Haijatajwa popote kwa Biblia.*
6. Nini ilifanyika wakati Yesu alizaliwa?  
*Roho Mtakatifu alimshukia Yesu na Mungu akasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, Ninayependezwa naye."*
7. Ni mambo gani matatu yenye Yesu alijaribiwa kufanya jangwani?  
*Fanya mawe iwe mikate, jitupe kutoka kwa kilele cha hekalu, jitawaze uwe mfalme.*
8. Kweli Yesu alijaribiwa kama sisi? Alikuwa na ugumu wa kufanya haki?  
*Ndiyo, Yesu alijaribiwa kama sisi kabisa. Alikuwa na ugumu wa kufanya haki.*
9. Yesu alifanya nini iliyomsaidia kuheba hayo majaribu?  
*Aliomba Mungu na akakumbuka maneno ya Mungu kutoka kwa Biblia.*
10. Yesu anatusaidia namna gani kuheba majaribu yetu?  
*Anatuomba kwa Mungu atusamehe. Anataelewa vile tunajihizi.*

### Mistari ya kukariri

Luka 1:35      Mathayo 3:16 – 17      Waebrania 4:14 – 15      Waebrania 5:7 – 8

### Mazungumzo

Jinsi gani Yesu ni Mwana wa Mungu tena Mwana wa binadamu? Tunajuaje yeye si Mungu Mwana?

### Kuandika

Soma Mathayo 4:1 – 11. Andika majaribu matatu ya Yesu na maneno kutoka kwa Biblia yaliyomsaidia kuyaheba.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



## Somo la 31 Kuja kwa Mfalme – Yesu

**SOMA** Luka 1:26 – 35; Mathayo 3:13 – 17; Mathayo 4:1 – 11

### SOMO

Tangu wakati Koreshi aliruhusu watu wa Israeli warudi kwa nchi yao mpaka Yesu alipozaliwa ni zaidi ya miaka 500. Watu wa Mungu sasa wanaitwa Wayahudi. Kwa huu muda wa miaka 500, Wayahudi hawakuwa na mfalme wao. Mungu aliwanyan'ganya ufalme kwa sababu watu wake walikuwa waovu. Mataifa mengine yaliwatawala. Wayahudi walijaribu sana kuwa huru lakini waliendelea kuwa chini ya mataifa yaliyotawala Mashariki ya Kati – Babeli, Wamedi na Waajemi, Yunani na Rumi sasawa na vile Mungu alionyesha Nebukadreza kwa ndoto.

Agano la Kale, Mungu alifanya ahadi nyingi sana kwa watu wake. Sasa wakati ulikuwa umetimia Mungu kutimiza ahadi zake.

### Ahadi za Mungu

<b>Adamu</b>	Mungu aliahidi kwamba mzao wake wa kipekee atashinda dhambi
<b>Ibrahimu</b>	Mungu aliahidi kwamba mzao wake wa kipekee ataleta furaha kwa watu wa mataifa yote.
<b>Daudi</b>	Mungu aliahidi kwamba mzao wake wa kipekee atakuwa mfalme kwa kiti cha enzi cha Daudi Yerusalemu. Atatawala juu ya Ufalme wa Mungu milele.
<b>Sedekia</b>	Mungu alimnyan'ganya Sedekia taji kwa sababu alikuwa muovu. Lakini Mungu aliahidi kwamba atampa mtu aliyehaki hiyo taji.

**Yesu anatumiza hizi ahadi zote**

Wayahudi wengi walijua ahadi zenye aliahidi. Walikuwa wameongoja Mfalme kutoka kwa uzao wa Daudi aje awape uhuru kutoka kwa Warumi. Walikuwa na habari ya mfalme waliyemtarajia. Alikuwa ni Masiya wao. 'Masiya' ni 'mpakwa mafuta.' Neno Masiya kwa Agano Jipya ni Kristo. Neno Kristo lina maana ya 'Mfalme'. Kila mara lina maanisha Yesu. Neno Yesu linamaanisha 'Mwokozi.' Yesu Kristo inamaanisha 'Mwokozi Mfalme'.

Yesu alikuja kutimiza hizi ahadi zote. Yesu alikuja kushinda dhambi. Alikuwa kuleta furaha kwa watu wa mataifa yote. Analeta tumaini la wokovu kwa Ufalme wa Mungu wa ajabu. Yesu aliishi maishi ya haki. Mungu atampa taji ili aje kuwa mfalme wa watu wa Mungu. Yesu atakuwa Mfalme kwa kiti cha enzi cha Daudi kule Yerusalemu. Atatawala Ufalme wa Mungu hapa duniani milele.

Mwishowe, wakati ulifika wa Mfalme kukuja na hadithi ya Agano Jipya ikaanza. Angalia mstari wa kwanza wa Agano Jipya. Inatwambia vile Yesu alikuja kutimiza ahadi zenye Mungu alisema kwa Agano la Kale. Yesu ni mzao wa kipekee mwenye Mungu aliahidi Ibrahimu na Daudi. Malaika Gabrieli aliambia Mariamu kwamba mwanawe, Yesu atakuwa Mfalme kwa kiti cha enzi cha Daudi na Ufalme wake utadumu milele. Yesu ni Masiya mwenye Mungu aliahidi. (Luka 1:32- 33).

Si ajabu malaika walifurahi na kushangilia wakati Yesu alizaliwa! Malaika waliimba, “Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowarithia.” Ahadi za Mungu zilikuwa zinatimizwa kwa kuzaliwa kwa Yesu.

Yesu alizaliwa kwa mama yake Mariamu kupitia kwa nguvu za Roho Mtakatifu. (Luka 1:35). Baada ya miezi tisa, Yesu alizaliwa. Yesu hakukuweko kabla ya kuzaliwa kwake. Yesu alizaliwa na kuanza kuishi kama wanadamu wengine wanapoishi. Ingawaje kuzaliwa kwake kulikuwa kwa kipekee kwa sababu Mariamu alikuwa bado bikira. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu.

Yusufu alikuwa mme wa Mariamu. Lakini Yusufu hakukuwa baba wa Yesu. Yusufu hakutimiliza ndoa mpaka Yesu alipozaliwa. Mungu alikuwa Baba wa Yesu. Yusufu alisaidia Mariamu kulea Yesu.

Yesu alikuwa Mwana wa kipekee. Yeye ndiye Masiya mwenye Mungu aliahidi. Yesu ndiye mzao asiyekuwa wa kawaida mwenye alikuja kutimiza ahadi za Mungu zote. Mungu alikuwa ameahidi huyu mzao wa kipekee kwa Adamu na Hawa, kwa Ibrahimu na Daudi. Mariamu alikuwa mzao wa hawa watu. Yesu alikuwa mwana wa Mariamu. Kutoka kwa Agano la Kale, Yesu ni mzao wa hawa watu. Yesu alikuwa mwanadamu. Alikuwa mzao wa laini ya kibinadamu.

Yesu alikuwa mwana wa Mungu. HAKUKUWA Mungu mwana. Hakuna mahali penye Biblia inasema Mungu mwana. Haya yalikuwa mawazo yaliyobuniwa tu na Kanisa la Wakristo saidi ya miaka nyingi baada ya Yesu kwenda Mbinguni. Neno Mungu Mwana halijafundishwa kwa Biblia. Yesu ni Mwana wa Mungu. Yesu hakukuweko kama mwanadamu kabla hajazaliwa Bethlehemu. Mungu alijua tangu mwanzoni kwamba atatuma Yesu aje. Mungu alikuwa na ahadi nyingi juu ya Yesu tangu wakati wa Adamu na Hawa. Yesu ni sehemu ya kusudi na ahadi za Mungu tangu mwanzo. Lakini Yesu hakukuweko mpaka alipozaliwa na Mariamu.

Tena Yesu alikuwa Mwana wa mtu. Yesu alikuwa mwanadamu kama sisi kwa sababu ya mama yake Mariamu. Yesu alikuwa na furaha hata huzuni kama sisi. Alikuwa na njaa na kiu kama sisi. Alijaribiwa kutenda dhambi kama sisi. Alikuwa mzao wa Adamu kama sisi. Lakini tena Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Mungu alikuwa Baba yake. Yesu alikuwa na tabia kama ya Mungu.

Yesu alikaa Nazareti na wazazi wake mpaka alipofika miaka 30. Binamuye, Yohana mbatizaji, alifundisha watu kwamba Masiya anakuja. Watu wengi walisikiliza Yohana. Yohana aliwabatiza kwa Mto wa Yordani kuonyesha kwamba walikuwa wametubu dhambi zao na wanataka kuishi maisha mazuri.

Siku moja Yesu alikuja kwa Yohana. Yohana aliambia Yesu kwamba hakutakiwa kubatizwa kwa sababu hakukuwa amefanya dhambi. Lakini Yesu alimwambia ambatize kwa sababu ilikuwa amri kutoka kwa Mungu. Yesu alipotoka majini, hua alikuja na kukaa kwa kichwa chake. Hii ilikuwa ishara kwamba Mungu alikuwa amempa Yesu nguvu zake, yaani Roho Mtakatifu. Kutoka mbinguni, Mungu alizungumza na Yesu, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.” Hii ilikuwa mwanzo wa miaka mitatu ya kazi ya Yesu ya kufundisha watu wa Mungu.

Mara tu baada ya kubatizwa, Mungu aliongoza Yesu mpaka nyikani ili ajaribiwe kwa siku 40. Yesu alikuwa na kazi kubwa ya kufanya. Ilitakiwa imani yake ijaribiwe na kuonyesha uaminivu wake kwa Mungu.

Yesu alijaribiwa lakini nguvu za Mungu zilimsaidia. Alijaribiwa eti abadilishe mawe iwe mkate kwa sababu alikuwa na njaa. Alijaribiwa kujitupa chini kutoka kwa kinara kirefu cha hekalu eti malaika watamwoko. Halafu watu watajua kwamba ana nguvu za Mungu na watamkubali yeye kwamba ni Masiya. Alijaribiwa eti atumie nguvu ya Mungu na kujitawaza kama mfalme. Yesu alishinda hayo majaribu yote kwa kukumbuka maneno la Mungu kutoka kwa Biblia. Mungu alifurahi sana kwa sababu Yesu alimpenda na kumtii.

Yesu alikuwa na hali ya ubinadamu kama sisi. Alijaribiwa sawasawa na vile sisi tunajaribiwa. Alitaka kufanya makosa. Ilikuwa vigumu sana kufanya mazuri. Wakati wote alifanya mazuri, ingawaje ilikuwa vigumu lakini alijaribu na kufaulu. Yesu alichukua muda mrefu akiomba Mungu amsaidie ili ashinde majaribio yake. Yesu HAKUKUWA Mungu. Mungu hawezi kujaribiwa. Mungu hawezi kutenda dhambi wala kufa. Yesu alijaribiwa kweli. Ilikuwa vigumu sana asifanye dhambi alipojaribiwa. Yesu alipigana vita kubwa sana, kushindana na dhambi lakini alishinda yote. Ndani yake, Yesu alishinda nguvu za dhambi.